**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021-2022

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW), mwingi wa Rehma, Muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia hali ya uzima na afya njema na kutuwezesha kufika hapa leo hii tukiwa katika hali ya utulivu na amani na kuweza kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** ninamshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano mkubwa, hali ambayo imeendelea kuipa nafasi Serikali na wananchi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Napenda kuwasisitiza viongozi pamoja na wananchi kwa ujumla tuendelee kudumisha kikamilifu amani na utulivu tulionao kwani bila ya amani na utulivu hakuna maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza na kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake, pia kujali

kwake Utawala wa Sheria na Utawala Bora katika kipindi chote tokea ashike hatamu ya kuiongoza nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha muhtasari wa Ripoti ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ripoti ambayo inaonesha shughuli zetu zote ambazo tumezitekeleza katika kipindi kilichopita.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambayo imeundwa na kupewa majukumu kwa mujibu wa kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Kanuni ya 107 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka 2020. Aidha, majukumu ya Kamati hii, yameelezwa katika jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la Mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti hii inaakisi kazi zote za Kamati ambazo zimefanywa kuhusiana na utekelezaji wa Taasisi ambazo zipo chini yake kwa kipindi cha mwaka wa fedha, 2021/2022 na kwa kuzingatia Mipango mikuu ya Kitaifa ambayo inajumuisha Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 – 2025.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufuatilia utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za maendeleo, Kamati hii imekuwa ikizisimamia Taasisi kuu Nne za Serikali ambazo ni OR – Katiba, sheria, Utumishi na Utawala Bora; OR – Tawala za Mikoa, serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ; Ofisi ya

Makamu wa Kwanza wa Rais; na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika,** Shukurani za pekee ziwaendee Wajumbe wa Kamati kwa mashirikiano yao makubwa ambayo yameiwezesha Kamati yetu kufanya kazi zake kwa ufanisi na uzoefu mkubwa na hatimae kukamilika kwa Ripoti hii. Napenda sasa niwatambue kwa majina Wajumbe wanaounda kamati hii kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Machano Othman said | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Suleiman Makame ali | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Zaina Abdalla salum | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *8* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *9.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *10.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

## MAUDHUI YA KAZI ZA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA:

**Mheshimiwa Spika,** Katika sehemu hii, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeelezea Utekelezaji wa shughuli za Wizara zilizofanywa kwa upana ambazo zinazosimamiwa na Kamati hii kwa kupokea taarifa tofauti za kila robo ya mwaka (quarterly reports) za utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara, kupokea taarifa za utekelezaji wa Maagizo ya Kamati, kukutana na wadau mbali mbali wa

sekta zinazosimamiwa na Kamati pamoja na kukagua baadhi ya maeneo na miradi mbali mbali ili kuona hatua za utekelezaji zilizofikiwa pamoja na kazi ya kupitia Miswada ya Sheria.

**Mheshmiwa Spika,** Aidha, Kamati ilifanya kazi zake za mizunguuko mitatu (3) kwa muda wa wiki Tisa (09) katika utaratibu iliojipangia kwa Unguja, Pemba na Tanzania Bara. Kadhalika, kupitia ripoti hii kamati imeibua changamoto zilizopo kwa Taasisi za Kiserikali pamoja na kutoa maoni na ushauri wa kuzitatua changamoto hizo kama ifuatavyo:

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KUU OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:

**Mheshimiwa Spika,** Katika Sehemu hii, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inasimamia masuala ya kupitia taasisi zake, kwa kuhusisha zaidi Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa haki, Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria, Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai, Programu ya Usimamizi wa Mapito ya Sheria na Programu ya Usimamizi wa Masuala ya dini. Programu hizi zinatekelezwa kupitia Mahkama Kuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria, Ofisi ya Mufti, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Idara ya Msaada wa Kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati wakati ikitembelea na kupokea taarifa za Mahkama imebaini ongezeko kubwa la kesi za udhalilishaji ambazo msingi wake ni kukithiri kwa matukio ya ubakaji, utoroshaji, ulawiti wa watoto na mengine mengi yenye mnasaba na hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Hivyo, Kamati inashauri Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya DPP na Mahakama Kuu kushirikiana kwa pamoja na kuangalia njia sahihi ya kuzipunguza kesi hizi pamoja na kupunguza mrundikano wa kesi za udhalilishaji kwa kuangalia madhaifu yaliyomo katika sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 2 ya Mwaka 2018 kwa kufanyiwa marekebisho suala la umri wa mtoto kuanzia miaka 15 mpaka 17 ambaye anatenda kosa la udhalilishaji kwa makusudi na kutiwa hatiani kwa mtoto wa kiume bila ya kuzingatiwa kuwa mtoto wa kike wameshirikiana kwa pamoja kutenda kosa hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imebaini kuwepo kwa changamoto ya majengo mabovu, yasiyoridhisha na ni hatarishi kwa maisha ya watu katika Mahkama zetu za Mikoa, jambo ambalo linapunguza ufanisi wa kazi zinazotekelezwa katika Mahakama hizo. Mfano mmoja wapo ni Mahakama ya Wete na Mahkama Mkokotoni. Kamati inashauri Serikali kuandaa mpango maalumu ambao utaiwezesha Mahakama kujenga upya Mahakama hizi pamoja na kuzifanyia ukarabati Mahakama zote zenye kadhia kama hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati wakati ikiendelea na utaratibu wa kuzipitia taasisi zake, kwa masikitiko makubwa imekua ikipokea malalamiko ya uchelewaji wa Mikataba inayopelekwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo hupelekea taasisi hizo kushindwa kuendelea na utekezaji wa kazi wanazozikusudia. Kamati imebaini kwamba Mikataba Mingi inayotoka katika Wizara au Taasisi husika haitayarishwi vizuri na hivyo kuifanya Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuwa na kazi nzito za kupitia Mikataba hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, uharaka wa baadhi ya Taaisi wa kutaka kurejeshewa Mikataba yao mara tu wanapoipeleka inapelekea utekelezaji

wa kazi zao kuwa ngumu. Kamati inaishauri Serikali pamoja na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuandaa mafunzo maalumu ya uandishi wa mikataba kwa wanasheria wa taasisi zote na wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inapendekeza Wizara na Taasisi zake kuwa na utamaduni wa kuipitia Mikataba yao kwa kuwatumia ipasavyo Wanasheria wao na kujiridhisha kabla ya kuipeleka Mikataba hiyo katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu, kufanya hivyo kutasaidia Mikataba kupatikana kwa haraka na yenye viwango bora zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** wengi wetu tunafahamu kwamba **Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka** inasimamia Kituo cha Huduma za Sheria na Utafiti (Zanzibar Law Resorce Centre) ambacho bado kinahitaji uangalizi wa hali ya juu ili kuenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya Sheria yatayokidhi haja kwa wazanzibari na Afrika Mashariki kwa ujumla. Kwa msingi huo Kamati inashauri Afisi ya DPP kukitangaza Kituo katika vyanzo mbali mbali vya habari ili jamii ya wanafunzi na watumishi wa umma watambue uwepo wa kituo hiki hapa Zanzibar pamoja na umuhimu wake katika sekta ya sheria kwa kwenda sambamba na mitaala ya kitaifa na kimataifa ili kutoa wanafunzi bora ambao watahudumu katika sekta za sheria kwa nchi zote za ukanda wa Afrika mashariki na Kati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa **Tume ya Kurekebisha Sheria** Kamati inaishauri Wizara na Taasisi husika kufanya utafiti wa kina wa sheria za miaka mingi tangu kutungwa kwake pamoja na zile ambazo utekelezaji wake umekua ukiibua migogoro baada ya kuitatua. Kamati inashauri Tume kuzikumbusha taasisi za Serikali juu ya umuhimu wa kuzifanyia marekebisho sheria zake hasa zile ambazo tayari

wameshazipatia utafiti ikiwemo Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam. 10 ya Mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Sekta ya Utumishi wa Umma, Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa wafanyakazi katika taasisi mbali mbali pamoja na utaratibu wa kuazima wafanyakazi kutoka taasisi nyengine unaoendelea, lakini pia kuna vijana wengi ambao wamemaliza masomo yao na wanahitaji ajira hasa walimu na madaktari.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kuweka mpango maalumu wa kuajiri watendaji wapya pamoja na kuzitembelea Taasisi za Umma na kufanya ukaguzi kwa watumishi ili kugundua changamoto za uhaba wa watumishi katika Taasisi hizo ukizingatia shughuli za uhakiki zimekamilika na vile vile, kuwepo kwa ongezeko kubwa la wanafunzi wa shule za msingi na sekondari bila ya kuwepo kwa walimu wa kutosha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma, Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la Miundo ya Taasisi katika baadhi ya taasisi za umma ikiwemo Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, na Wakala wa Serikali Mtandao, miundo ambayo haijakaa sawa na kusababisha waajiriwa kutojua madaraja yao ya kazi pamoja na majukumu yao kiujumla. Kamati inashauri Serikali na taasisi husika kuharakisha suala la upatikanaji wa miundo ili wafanyakazi hao waweze kujua nafasi zao kwa mujibu wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile kwa upande wa Serikali Mtandao, kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya Muundo wa Wakala licha ya kuandaa muundo wao na kuuwasilisha katika mamlaka husika kwa kuidhinishwa, bado Wakala imechelewa sana kupata muundo wa

kiuendeshaji tangu ilipoanzishwa mwaka 2019. Aidha, kuwepo kwa tatizo la upatikanaji wa fedha kwa Wakala ambapo hupangiwa bajeti ndogo na haitoshi kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Wakala bado haina ruzuku hadi sasa na matokeo yake ruzuku za Wakala zinapitia kwenye fungu la Katibu Mkuu. Hivyo, Kamati inashauri kuwezeshwa kwa Wakala ambao umeonekana kuwa kimya katika utekelezaji wake kutokana na ukosefu wa fedha za matumizi. Ni jambo la kusikitisha kuona hadi leo baadhi ya taasisi za Serikali kama vile Hospitali zinaagiza wagonjwa wao kutumia mabuku badala ya kutumia mifumo ya kisasa ambayo hutumika kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za wagonjwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwepo kwa baadhi ya Taasisi ambazo haziwafanyii wafanyakazi wake wapya mafunzo ya awali (induction course) kwa wakati unaostahili hivyo, kupelekea Tume ya Utumishi wa Umma kushindwa kuwathibitisha kwa wakati. Kamati inashauri Tume kufuatilia moja kwa moja katikaTaasisi za Umma ili kubaini Taasisi ambazo zinachelewesha watumishi wao kuwafanyia mafunzo ya awali na kuwachukulia hatua za kinidhamu wakuu wa Taasisi hizo ambao hawatekelezi agizo hilo kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014.

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ina jukumu la kusimamia Sera, Sheria na Kanuni za Ofisi ili kuhakikisha kuwa inaweka mazingira mazuri ya kutoa huduma za kijamii na kiuchumi na vile vile kuimarisha ulinzi na usalama kwa wananchi na wageni wanaoingia na kutoka Zanzibar. Aidha, Ofisi hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli zinazotekelezwa na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo zinasaidia kupunguza umasikini na kukuza uchumi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaipongeza Serikali kwa kuja na uamuzi wa kujenga masoko ya kisasa yatayoendana na wakati katika mji wetu wa Zanzibar katika maeneo ya Mwanakwerekwe, Chuini, Jumbi pamoja na Bazar katika maeneo ya Darajani. Hata hivyo, Kamati imepata wasiwasi baada ya Mkandarasi kutoa maelezo ya mradi wa Maduka ya Darajani ambayo yatajumuisha Maduka yenye ukubwa tofauti, ofisi mbali mbali zitazojengwa eneo la skuli ya Vikokitoni na Darajani bila ya kuwepo eneo la kuegesha magari kwa wale wote wataofika kufanya manunuzi katika eneo hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inashauri na kuiomba Serikali kuangalia upya uwezekano wa kutenga eneo la kuegesha magari japo kwa skuli ya Vikokotoni na skuli ya Darajani kubaki Ofisi wanazozitarajia. Kufanya hivyo kutakuwa kumelenga kuwasaidia watu wenye mahitaji maalumu, wafanya biashara ambao watakuwa maeneo hayo muda mwingi pamoja wanunuzi wa ndani na nje ya nchi ambao watarahisishiwa kubeba mizigo yao na kutembea masafa ya karibu zaidi. Kamati inasisitiza Serikali kuangalia umuhimu wa kuwa na sehemu ya maegesho ya magari katika eneo la skuli ya Vikokotoni.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha hali ya ulinzi na usalama kwa Mikoa yetu, Kamati inasikitishwa na kuibuka upya kwa vitendo vya wizi na kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu katika maeneo mbali mbali ya miji ambavyo vinafanywa dhidi ya raia na mali zao vinavyotokea kila siku na kuhatarisha maisha ya wananchi. Vitendo hivyo ni kama vile, kupigwa watu mapanga, wizi uliokithiri, kunyang'anywa watu mali zao, ongezeko la madada poa waliozagaa katika Mikoa yetu ya Unguja na Pemba. Kamati inashauri uongozi wa Mikoa yote yenye kadhia kama hizi kutoyafumbia macho maovu haya kwa kuwachukulia hatua kali wahusika wote wa vitendo hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hayo, kumekuwa na hujuma za makusudi kwa mioundombinu ya Serikali kwa ujumla, kama vile wizi mkubwa wa miundombinu ya visima vya maji maeneo ya Bumbwi sudi Unguja na maeneo ya Gae la Mtungi kwa upande wa Pemba pamoja na wizi mkubwa uliofanyika wa nyaya za taa za barabarani katika barabara ya "Mkapa road" na hivyo kupelekea barabara hiyo yenye nafasi kubwa ya kuleta maendeleo kushindwa kuimarika na hakuna hatua endelevu zinazochukuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaiomba Serikali kulisimamia suala hili ipasavyo kwa kuwa imetumia pesa nyingi kutekeleza miradi hii na haipendezi kuona wasiopenda maendeleo pamoja na wanaonunuwa nyaya za umeme ambao wameshasababisha kuhujumiwa kwa miundombinu ya taa za barabarani na kutia hasara Serikali katika uimarishaji wa miji yetu. Aidha, Kamati inaiomba Serikali kupiga marufuku ununuzi wa nyaya chakavu za umeme kwa maeneo yote ya Zanzibar mpaka suala hili litakapo patiwa ufumbuzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imegundua uwepo wa tatizo la kimuundo ambalo lipo katika utekelezaji wa kazi za majukumu ya Baraza la Manispaa ya Mjini, Baraza la Manispaa ya Magharibi A, Baraza la Manispaa ya Magharibi B na Baraza la Jiji la Zanzibar ambapo licha ya muundo lakini hata katika mipaka ya kimaeneo na utawala bado ipo changamoto na inahitaji kupatiwa ufumbuzi wa kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** ili kufikia malengo na dhamira nzuri ya Serikali katika kuanzisha Mabaraza haya basi ni vyema marekebisho ya Sheria Namba 7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikafanyiwa marekebisho na ukawepo muundo mmoja kwa Zanzibar

ambao utaainisha Baraza la Jiji la Zanzibar na Baraza la Manispaa ya Magharibi A na Magharibi B kwa kuzingatia mipaka ya kijiografia, kazi zake pamoja vyanzo vya mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, imebaini kuwepo kwa mgongano wa kimaslahi kati ya Mamlaka ya Mji Mkongwe na Baraza la Manispaa ya Mjini kutokana na muingiliano wa majukumu ya kazi zao kama vile ukusanyaji wa mapato, utoaji wa vibali vya biashara na makatazo mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya “Data base” ya wafanya biashara wanaotumika kuchangia mapato katika Mabaraza yote kwa Unguja na Pemba jambo linalopelekea kutokuwa na data za uhakika za walipaji wao wangapi, wako wapi na nikina nani hali inayosababisha kodi kupotea na kukosekana kwa makisio halisi ya ukusanyaji wa mapato. Kamati inashauri Mabaraza ya Manispaa na Halmashauri zote kuanzisha mfumo maalumu utakaowasaidia kujua idadi ya wafanyabiashara pamoja kiwango cha mapato ambacho kitakadiriwa kwa uhalisia wa wafanyabiashara waliopo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia katika ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ya Mabaraza na Halmashari imebaini kuwepo kwa usimamizi usioridhisha wa miradi ambayo hupelekea pesa nyingi zinazokusanywa na halmashauri hazitumiki kimalengo ya miradi au Diwani mmoja kupewa miradi mingi zaidi ili aweze kunyamaza au fedha za miradi kutumika katika matumizi mengineyo na hivyo kupelekea miradi isiyo na ufanisi na kuikosesha jamii na Serikali kufikia malengo yaliyokusudiwa. Hivyo, Kamati inashauri wakati Taasisi hizi zinapoanzisha miradi yake ya kimaendeleo kuwepo usimamizi

madhubuti na wa kitaalamu ambao utapelekea ubora wa mradi unaotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikufurahishwa na baadhi ya Halmashauri na Mabaraza kupitia wakurugenzi wa Manispaa kwa Unguja na Pemba wanawanyanyasa, kuwasumbua na kuwadharau waheshimiwa Madiwani bila kujali kwamba wamechaguliwa na wananchi na wamepewa nafasi hiyo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kupitia uchaguzi mkuu wa nchi hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haipendezeshwi na tabia ya kuona mtendaji wa Serikali anapotosha maadili yake na kwenda kinyume na mamlaka ya uteuzi ambayo imempa jukumu la kuwa msimamizi wa Taasisi hizi za umma. Hivyo, Kamati inawashauri wakurugenzi wote wenye tabia hii kuacha mara moja tabia ya kuwanyanyasa Madiwani na kuona kwamba hawa ni sehemu ya viongozi ambao wamechaguliwa kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Kamati inashauri Serikali posho lao wanalowalipa Madiwani liwe linatoka Serikali Kuu.

**Mheshimiwa Spika,** tatizo la wafanyakazi wa Mikataba wa Halmashauri ambao wameshaitumikia Serikali kwa muda mrefu na mwisho wake wamesimamishwa kazi bila ya kujua hatma yao imekuwa ni suala nyeti hapa Zanzibar. Kamati inaamini kwamba zipo sekta muhimu lazima zipatiwe wafanyakazi wa mikataba kama viwanja vya ndege, bandarini na katika Manispaa za Miji. Kamati inashauri Tume ya Utumishi Serikalini kuishauri Serikali kuwarudisha wafanyakazi wote wa Mkataba ambao wamesimamishwa bila ya kujua hatma yao ya kimaisha.

**Mheshimiwa Spika,** wafanyakazi hawa wana kila sababu ya kurejeshwa kutokana na uzoefu wao katika maeneo yao ya kazi. Hivyo, ni jukumu la

Serikali kulipa kipaumbele suala hili kwa kutumia busara zaidi. Aidha, Kamati inashauri Tume kutoa uelewa kwa watumishi juu ya mikataba ya kazi pamoja na mambo yote muhimu yanayohusiana na utumishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa **Idara Maalumu za SMZ,** Kamati imefurahishwa na kasi ya uanzishaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Idara Maalumu za SMZ kama agizo la Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dokta Hussein Ali Mwinyi lililowataka wakuu wa vikosi kuanzisha miradi ya uzalishaji ili kupunguza utegemezi wa Serikali na kusimamia rasilimali fedha zilizokuwepo kwenye vikosi.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia nafasi hii, Kamati inampongeza Komodoo Mkuu wa Kikosi cha KMKM kwa kulitekeleza vyema agizo hili kwa kuweza kutafuta wawekezaji na kuanzisha miradi mingi ya kimaendeleo kama vile kuwa na meli ya uvuvi na kuanza kuvua katika bahari kuu, kuanzisha bekari na kuanzisha mfumo wa malipo kwa njia ya kielektroniki katika hospitali ya KMKM Kibweni ili kudhibiti upotevu wa mapato. Kamati inashauri Vikosi vyote vya SMZ kuiga mfano wa Kikosi cha KMKM kwa kuanza kubuni miradi mbali mbali na kutafuta wawekezaji ili kujiimarisha kimaendeleo na kuwaongezea kipato ili kuondokana na utegemezi Serikalini. Aidha, Kamati imeona kwamba ipo haja kwa Vikosi vyote ambavyo vinategemea kuanzisha miradi kukaa na wataalamu wa Serikali na kuona miradi yao wanayotarajia kuitekeleza italeta tija na haitaleta madhara kwa nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza juhudi za Jeshi la Kujenga Uchumi kwa busara zao za kuongeza majengo ya kituo cha afya kilichopo Saateni kutokana na kuona umuhimu wake, ambapo mbali ya kutumiwa na askari lakini pia wananchi kutoka sehemu mbali mbali

wanatumia kituo hiki. Kamati inashauri JKU kumaliza ujenzi wa kituo hiki kwa haraka ili kupunguza msongomano wa wagonjwa katika majengo yaliyopo kutokana na idadi kubwa ya wagonjwa wanaofika kituoni hapo kwa ajili ya kupatiwa huduma za matibabu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika ziara zake za Jeshi la Kujenga Uchumi ilifika katika Kambi ya Bambi Kim na kukagua maendeleo ya uzalishaji katika sekta ya kilimo na mifugo na kuona namna wanavyosaidia vijana kuwapatia mafunzo ya kazi za amali katika shughuli mbali mbali. Aidha, Kamati ilionana na kupokea taarifa ya muwekezaji wa kilimo kutoka nchini Misri ambae amekuwa akitumia shamba la JKU kwa shughuli zake za uwekezaji katika sekta ya kilimo huku nyenzo anazotumia anapatiwa na JKU, wahudumu, madereva, wapishi na walinzi wote hao wanatoka JKU bila ya kulipia fidia yoyote.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto nyingi zilizokuwepo kwa muwekezaji huyu, Kamati inaishauri Serikali ikiwa kuna Mkataba ambao umefungwa na muwekezaji huyu basi usitishwe mara moja na ikiwa hapana mkataba maalum wenye manufaa kwa pande zote mbili basi Serikali imuondoe muwekezaji huyu ili kutoa fursa kwa mashamba hayo kutumiwa na JKU kwa kazi zao za uzalishaji pamoja na kuwapunguzia mzigo wa hasara inayopatikana kwa kikosi lakini pia hakuna faida yoyote ya nchi au jamii iliyotoa mashamba haya kwa muda wote wa miongo iliyopita.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inapenda kushauri Serikali na Vikosi vyetu kutekeleza majukumu ya uzalishaji kwa mujibu wa muundo na sheria za kikosi husika ili kuvipa nguvu katika uzalishaji wake. Aidha, Tunaiomba Serikali kuvipa vyenzo vikosi hivyo kwa kuwa, wakuu wa vikosi wanakiri kama watapewa nyenzo kama pembejeo za kilimo kwa JKU na Magereza,

na kwa upande wa KVZ wakipatiwa vifaa kamili vya Ulinzi basi wataweza kujiendesha wenyewe bila ya kuitegemea Serikali kwa ruzuku. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuzipitia sheria Nam. 6 ya Mwaka 2003 ya JKU na Sheria Nam. 4 ya Mwaka 2004 ya KVZ na kutafuta namna ya kuwagawia majukumu ya kazi za ulinzi kwa vikosi vyote viwili.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, imebaini kuwepo kwa changamoto ya muda mrefu katika Idara Maalumu kwa kukosa hati za umiliki wa maeneo yao na hivyo, kupelekea kuvamiwa na wananchi au Taasisi nyengine za Serikali. Aidha, Kamati inasikitishwa na kuona zipo Idara ambazo zimeshakamilisha utaratibu wa kupatiwa hati lakini hadi leo imeshindikana kpimiwa na kupatiwa hati zao kwa mujibu wa utaratibu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepata vielelezo vya kutosha vinavyoonesha jinsi kikosi cha Valantia Zanzibar kilivyofuatilia suala hili na hatima yake kushindwa kupimiwa maeneo yao ambayo tayari yalishalipiwa tokea mwaka 2011 na mwaka 2018 licha ya kukumbushia kila baada ya muda mfupi. Kamati inaiyomba Serikali kuingilia kati changamoto hii kwa kuagiza Taasisi inayohusika na upimaji kutekeleza vyema majukumu yake kwa kuzingatia umuhimu wa Taasisi zenyewe ili kupunguza changamoto za ardhi zinazojitokeza siku hadi siku na kutia aibu kwa vikosi hivi vya kijeshi kugombana na wananchi kwa sababu ya mipaka ambayo haikupimwa kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, kapitia Idara Maalumu, Kamati imebaini kuwepo kwa, ukosefu wa Mahanga na nyumba za Wakuu wa vikosi kwa baadhi ya vikosi kama vile kikosi cha KMKM Tundauwa Pemba kutumia banda moja kwa makaazi ambalo haliridhishi. Aidha, huduma za matibabu ya uhakika kwa baadhi ya vituo vya afya zinakosekana kwa kuwa Vituo hivyo havikidhi mahitaji ya askari wake, huku tukizingatia

wananchi wanaozunguuka maeneo hayo wanategemea kupata huduma za afya kupitia vituo hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya usafiri kwa makamanda na maafisa waandamizi wa vikosi vya SMZ. Kamati inaishauri Serikali yetu Tukufu kuliangalia kwa kina suala hili na kulipatia ufumbuzi kwani Askari wetu wanadhalilika kwa kutegemea usafiri wa kijamii. Sambamba na hilo, Kamati inapendekeza kwa Serikali kuanzisha utaratibu maalumu wa kutoa vyombo vya usafiri kwa njia ya mkopo wenye masharti nafuu ambao utawawezesha askari wetu kumiliki vyombo hivyo ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, Kamati inashauri Serikali kuangalia namna ya kuwasaidia Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ambacho kinafanya kazi Viwanja vya ndege na Bandarini kupata stahiki zao za muda mrefu kutoka kwa Mamlaka husika kwa lengo la kuimarisha malengo ya kikosi hiki pamoja na kuwatia ari ya kufanya kazi askari hao wa uwokozi.

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilirejea rasmi mwezi wa Disemba, 2020 ambapo inashughulika na masuala mtambuka ya uhifadhi, usimamizi na utunzaji wa mazingira, masuala ya watu wenye ulemavu, masuala ya VVU na UKIMWI na masuala yanayohusu udhibiti wa dawa za kulevya. Ofisi hii pia inasimamia na kuratibu Ofisi ya faragha ya Makamu wa Kwanza wa Rais, pamoja na masuala ya Sera, Mipango na Tafiti za Ofisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kutokana na juhudi zake za uhifadhi wa mazingira yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi, kama vile eneo la ufukwe wa bahari ya Msuka kwa kujenga ukuta ambao utazuia athari kwa mmong'onyoko unaotokana na maji ya Chumvi. Tunaiomba Serikali kuendelea na utaratibu wa kuhifadhi maeneo mengine ya bahari kwa namna kama hiyo pamoja na kuelimisha wananchi namna ya kulinda maeneo hayo ili athari zisijekuendelea zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** tunasikitishwa kuona kwamba Zanzibar ni nchi ya visiwa lakini imekuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira kama vile uchimbaji wa kifusi na mchanga, mifuko ya plastiki inayouzwa hadharani, ukataji miti kiholela na uchomaji wa misitu, ufukiaji na uchomaji wa dawa na vyakula vilivyoisha muda wake kwa matumizi ya binadamu, huku utekelezaji wa Sheria yake unasuasua. Kamati inaishauri Serikali kuliangalia suala hili kwa umakini na ukaribu zaidi kwa kufuata sheria kikamilifu ili kupunguza athari za kimazingira na wananchi wanaoishi karibu na maeneo yanayotumika kuteketeza bidhaa hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia ofisi za watu wenye ulemavu, Kamati inapongeza kwa kuanzishwa kwa utaratibu wa "database" kwa ajili ya kuwatambua watu wenye mahitaji maalumu kuwaingiza kwa pamoja na kuwawekea miradi endelevu ya kuwawezesha kuwasaidia na kuwapatia vifaa visaidizi kama vile fimbo na vigari maalumu kwani tunaamini sisi sote ni walemavu watarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Sote tunakumbuka kwamba hivi karibuni, katika Baraza hili Tukufu tumepitisha Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya

ili kuzidisha mapambano juu ya biashara ya Dawa za kulevya hapa Zanzibar. Kamati inashauri utekelezaji wa Sheria hii mpya iwe na uweledi wa hali ya juu na mapambano dhidi ya janga hili lionekane kama ni mapambano ya Serikali kwa kuzihusisha Taasisi zote na kutowafumbia macho wale wote watakaopatikana na hatia a uuzaji, usafirishaji na uingizaji wa Dawa za Kulevya katika nchi yetu kwani Zanzibar bila dawa za kulevya inawezekana.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, imebaini mapambano dhidi ya maradhi ya UKIMWI yanatumika kama ni fursa ya kujipatia kipato badala ya kufanywa ni njia ya kutokomeza maradhi haya kutokana na kuanzishwa kwa jumuiya kadhaa ambazo zinahusika na mapambano ya UKIMWI ilhali ongezeko ni kubwa na jamii inaathirika. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mkakati maalumu utakao komesha biashara haramu ya ngono katika nchi yetu ambayo ndio chanzo kikuu cha maradhi haya. Aidha, jamii ifahamu kwamba mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI ni jukumu la kila mmoja, hivyo ni wajibu wetu kutojihusisha na vitendo vitakavyopelekea ongezeko la maambukizi mapya. Pamoja na hayo, Tume itafute vyanzo vipya vya mapato badala ya kutegemea wafadhili kutoka Mashirika ya Kimataifa ili kuongeza kasi ya kutokomeza maradhi haya.

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

**Mheshimiwa Spika,** majukumu makhsusi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Utaratibu na Baraza la Wawakilishi ni pamoja na kutoa huduma bora kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa; kuandaa na kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa; kuratibu masuala ya Muungano;

kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Tanzania Bara. Vile vile, inaratibu na kusimamia shughuli za Baraza la Wawakilishi na Tume ya Uchanguzi ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Ofisi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF kwa ujenzi wa Hospitali katika Shehia ya Nanguji Jimbo la Kiwani ambayo itakuwa na huduma za mama na mtoto pamoja na matibabu mengine, mradi wa ujenzi wa madarasa na uzio wa skuli ya Piki na mradi wa nyumba za maendeleo Kizimkazi. Hata hivyo, Kamati inashauri mfuko wa TASAF kuzidisha juhudi za kuzitambua kaya masikini kwa kufanya ufuatiliaji wa moja kwa moja majumbani ili kubaini wenye sifa za kuwa wanufaika wa mradi na kupunguza malalamiko kupitia program ya kuwasaidia wananchi juu ya miradi midogo midogo wanayoiibua vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati inaiomba Serikali kufanya mazungumzo na Makao Makuu ya TASAF Tanzania Bara ili kuanzisha ofisi ndogo ya TASAF hapa Zanzibar kwa lengo la kusaidia kutatua changamoto zinazojitokeza bila kuzifikisha makao makuu kama vile suala la mchanganyiko wa majina yanayofanana pamoja na kuwarudisha wale wote wanaotolewa katika mfumo kwa visingizio tofauti.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kujiandaa mapema katika kukabiliana na maafa badala ya kusubiri maafa kutokea ndio ikaanza hatua za kukabiliana nayo. Aidha, kwa upande wa Idara ya Sherehe na Mapambo, Kamati inashauri kuwekwa utaratibu mzuri wa upangaji wa viongozi katika sherehe za kiserekali zinapofanyika katika maeneo rasmi yaliyotengwa kwa ajili ya sherehe hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Baraza la Wawakilishi, Kamati inaishauri Serikali kuwapatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la Afisi ya Baraza ambalo litahusisha ofisi za watendaji na kumbi za Kamati. Kamati pia, inashauri katika ujenzi huo kuangalia suala zima la kuwepo kwa kituo kidogo cha afya ndani yake.

**HITIMISHO**:

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla wake Kamati yetu inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Taasisi zote ambazo zipo chini ya Kamati hii kutokana na mashirikiano yao makubwa wanayoyapata kutoka kwa viongozi wa Taasisi hizo, akiwemo Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohammed; Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum; Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Mwalim Haroun Ali Suleiman; Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, pamoja na Mhe. Masoud Ali Mohammed; Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaomba kuwashukuru Makatibu wakuu wote wa Taasisi hizi, Makamanda wa Idara Maalum, wakuu wa Mikoa na wakuu wa Wilaya wote wa Zanzibar kwa ushirikiano wao mkubwa walioipatia Kamati wakati wa kazi zake. Aidha, Kamati inawashukuru watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakiongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Ndugu Raya Issa Mselem kwa ushirikiano waliotupatia katika kufanikisha kazi za Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri viongozi wa Wizara na taasisi zote zinazosimamiwa na Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika mizunguuko ya ziara za Kamati, kutokufanya hivyo kutaipelekea Kamati kushindwa kupokea taarifa zao au kuzitembelea taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika,** imekuwa ni jambo la aibu kuona kila mizunguuko ya kamati inapofanyika kufuatia taarifa za utekelezaji wa fedha za bajeti kupokea changamoto endelevu ambazo zinachukua muda kufanyiwa kazi, kwa mfano: magari chakavu au ofisi kukosa gari kabisa, majengo kuwa chakavu au uhaba wa nafasi kwa watendaji hali inayopelekea kukosa ufanisi wa ufanyaji kazi kutofikia malengo. Kamati yangu inaishauri Serikali na Taasisi ambazo zinakumbwa na Changamoto hizi kutafuta njia mbadala za kuzitatua ili ifike muda Kamati zisikie changamoto nyengine kinyume na hizi.

**Mwisho Kabisa**, napenda niwaombe wajumbe wa Baraza hili Tukufu kuisoma, kuifahamu na kuichangia Ripoti hii ili Taasisi zilizoguswa kuweza kupokea ushauri na maoni ya wajumbe kwa lengo la kuyafanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika,** *Naomba Kutoa Hoja.*

Ahsante,

…………………………

(Mtumwa Peya Yussuf)
Makamu Mwenyekiti
Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa
**BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**